

Mafuta kwenye kondomu

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Mafuta yanayowekwa kwenye pakiti ya kondomu ni mafuta maalum na yana kazi ya kuhifadhi kondomu mpaka siku yake ya kutumiwa. Bila mafuta haya kondomu isingekuwa imara, ingekauka na isingekuwa nyumbufu vya kutosha. Vilevile mafuta hayo yanalainisha mpira ili kurahisisha uvaaji na matumizi yake. Kwa watu wengi, mafuta haya hayawaletei matatizo yoyote. Watu wachache sana ambao ngozi yao ni nyepesi kuathirika wanapata matatizo ya kuwasha baada ya kutumia kondomu.

Muwasho huwa sio wa kudumu. Watu wa namna hii wanashauriwa kunawa na sabuni ya kawaida baada ya kujamiiana. Kuna uvumi kwamba mafuta haya yaliyomo ndani ya pakiti ya kondomu yana virusi vya UKIMWI. Hii siyo kweli, mafuta hayo yanawekwa kwa ajili ya kuhakikisha uimara wa kondomu tu.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25746>